TANGAZO LA SERIKALI Na. 1007 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

SHERIA NDOGO YA KUDHIBITI OMBAOMBA YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"eneo la wazi" maana yake ni eneo lolote la ardhi lenye bustani au ambalo halijaendelezwa ambalo lipo kwa ajili ya matumizi ya umma;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

"kituo cha hifadhi" maana yake ni kituo, mahali au jengo lolote ambalo limetengwa au linatumika kuwahifadhi ombaomba, wazee, watoto au watu wenye ulemavu kwa lengo la kuwapa mahitaji ya msingi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mtaa" maana yake ni eneo lolote lililopo ndani ya Halmashauri na inajumuisha maeneo yote ya

barabara, hifadhi za barabara na njia ya waenda kwa miguu;

"ombaomba" maana yake ni mtu yeyote anayeishi kwa kutegemea kuomba chakula, fedha au vitu vingine kutoka kwa mtu mwingine kwenye mitaa, kando ya barabara na maeneo ya wazi yaliyoko ndani ya eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-
(a) kudhibiti ombaomba kwenye eneo lote la Halmashauri; na
(b) kuwatambua ombaomba.

Kutambuliwa kama ombaomba

5. Mtu yeyote atatambulika kuwa ombaomba endapo-
(a) atakutwa mtaani au kwenye eneo la wazi akiomba fedha au chakula kwa mtu au watu wengine; au
(b) atakutwa mtaani, kando ya barabara au kwenye maeneo ya wazi akiwa amekaa, amesimama au amelala akionesha vidonda au ulemavu kwa madhumuni ya kushawishi kupewa fedha au kuomba fedha.

Uteuzi wa Wakala

6. Halmashauri inaweza kumteua wakala ambaye atatekeleza jukumu la kudhibiti ombaomba kwenye sehemu au eneo lote la Halmashauri kwa niaba ya Halmashauri.

Taratibu za kuwakamata ombaomba

7.-(1) Mtu yeyote atakayekutwa mtaani au maeneo ya wazi akiomba fedha, chakula au kitu kingine chochote atakamatwa na kuchukuliwa taarifa zake muhimu ikiwemo-
(a) jina kamili;
(b) jinsi na umri;
(c) kijiji, wilaya na mkoa anaotoka; na

(2) Ombaomba atakayekamatwa atapigwa picha kwa ajili ya kumbukumbu, na picha hiyo itatumika kwa

matumizi ya ofisi ili kurahisisha utambuzi iwapo atarudia kuwa ombaomba.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kuwarejesha ombaomba waliokamatwa kwenye Mikoa wanayotoka na kuwakabidhisha kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika.

Makosa

8. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-
(a) ataomba na kupokea msaada wa fedha, chakula au kitu kingine chochote mtaani, kando ya barabara au kwenye maeneo ya wazi na mahali popote ambako siyo kituo cha hifadhi;
(b) atarudi na kuendelea kuombaomba katika Halmashauri baada ya kurejeshwa katika Mkoa aliotoka;
(c) atamtembeza mtu mwingine barabarani, mtaani au maeneo ya wazi kwa miguu au kwa kutumia chombo chochote kwa lengo la kuombaomba;
(d) atamsafirisha kutoka eneo moja hadi jingine mtu yeyote kwa lengo la kumtumia kuombaomba mtaani;
(e) atamtumikisha mtoto kwa shughuli za kuomba kwenye magari, barabarani, mtaani au mahali pengine popote; au
(f) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Adhabu

9. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa lolote kinyume cha Sheria Ndogo hii, atawajibika kilipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalum kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hii.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na. 529 la 2019

11. Sheria Ndogo ya Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ya Mwaka 2019 inafutwa.

______

JEDWALI

______

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, NINAKUBALI kulipa kiasi cha shilingi …………………….. kama faini ya kufifilisha kosa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………
Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YA MKURUGENZI:
Jina: …………………………………..………………………
Saini……………………….…………………………..………
Tarehe………………………………………………………….

Lakiri ya Jiji la Dar es Salaam imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutao wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam uliofanyika tarehe 6/3/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

JOMAARY MRISHO SATURA,<br>
*Mkurugenzi wa Jiji,*<br>
*Halmashauri ya jiji,*<br>
*Dar es salaam*

MHE. OMARY KUMBILAMOTO,<br>
*Msahiki meya,*<br>
*Halmashauri ya jiji,*<br>
*Dar es salaam*

**L.S**

**NAKUBALI**,

Dodoma,<br>
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,<br>
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*